**SUMAIT University Journal (SUJ)**
eissn (2953-2698)
Issue No.18 June 2026

# DHIMA ZA MITINDO YA LUGHA KATIKA MIJADALA YA BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR

**Asha Iddi Bavuai**
*E-mail address: ashaiddibavuai@gmail.com*

*Department of Kiswahili, School of Kiswahili and Foreign Languages.*
*State University of Zanzibar, Zanzibar, Tanzania*

*Received: January 2026, Accepted: April 20226, Published June 2026*
*© SUMAIT University Journal 20226*

**Abstract:**
*This article examined the functions of language styles in the debates of the Zanzibar House of Representatives (BLW). The objective of the article was to analyze the functions of language styles used in the debates of the BLW. The study was guided by the Theory of Language Functions established by [1], which explains that language functions as a social, psychological, and cognitive tool in legitimizing/legitimize authority and shaping relationships.The study employed the questionnaire method, with questionnaires used as instruments for data collection. Data analysis adopted an interpretive approach involving textual analysis of twelve (12) official Hansard records of parliamentary debates. In addition, the study involved a sample of twenty (20) participants, including ten (10) members of the House of Representatives and ten (10) Hansard writers. Members of the House of Representatives were selected because they are the primary users of language in parliamentary debates, while Hansard writers were selected because they are custodians of the debate transcripts. The findings of the study revealed that language use in the BLW is categorized into four major language styles, each serving a specific function in the conduct of parliamentary activities. The frozen style functions to strengthen national identity and legitimize legal procedures through repetitive formal expressions. The formal style maintains protocol, respect, and the legitimacy of governmental decisions through the use of legal and constitutional vocabulary. Meanwhile, the consultative style promotes institutional cooperation and public participation in policy-making processes. Lastly, the casual style is used to simplify the understanding of complex arguments, build social closeness, and reduce tension in debates through humor and figurative expressions. The article recommends that balance and proper integration of these language styles are essential tools for enhancing political communication and improving the effectiveness of this constitutional institution.*

***Keywords:*** *Language styles, Zanzibar House of Representatives, Theory of Language Functions, Political Communication, Sociolinguistics.*

**Ikisiri**
*Makala hii imechunguza dhima za mitindo ya lugha katika mijadala ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar (BLW). Lengo la makala hii lilikuwa ni* kuchambua dhima za mitindo ya lugha katika mijadala ya BLW. *Uchunguzi wa makala hii umeongozwa na Nadharia ya Dhima za Lugha iliyoasisiwa na [1], ambayo inaeleza kuwa lugha hutumika kama chombo cha kijamii, kisaikolojia, na kiakili katika kuhalalisha mamlaka na kuunda*

*mahusiano. Mbinu iliyotumika ni hojaji na dodoso kama zana ya kukusanya data. Uchambuzi ulitumia mkabala wa kitaamuli, ikihusisha uchambuzi wa matini wa Kumbukumbu rasmi za mijadala kumi na mbili (12). Aidha uchambuzi umehusisha sampuli ya watu ishirini (20), ambapo wajumbe wa BLW walikuwa kumi (10) na waandishi wa hansadi kumi (10). Wajumbe wa BLW walichaguliwa kwa kuwa ni watumiaji wakuu wa lugha katika mijadala, huku waandishi wa hansadi ndio wahifadhi wa matini ya mijadala hiyo. Matokeo ya utafiti yamebainisha kuwa matumizi ya lugha katika BLW yamegawanyika katika mitindo mikuu minne, ambapo kila mmoja una dhima mahususi kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Baraza. Mtindo usiobadilika hutekeleza dhima ya kuimarisha utambulisho wa kitaifa na kuhalalisha taratibu za kisheria kupitia kauli za kikanuni zinazojirudia. Mtindo rasmi unadumisha itifaki, heshima, na uhalali wa maamuzi ya kiserikali kwa kutumia msamiati wa kisheria na kikatiba. Wakati huo huo, mtindo wa mashauriano unahimiza ushirikiano wa kitaasisi na ushirikishwaji wa wananchi katika maamuzi ya kisera. Mwisho, mtindo wa kawaida unatumika kurahisisha uelewa wa hoja nzito, kujenga ukaribu wa kijamii, na kupunguza mvutano katika mjadala kupitia utani na sitiari. Makala inapendekeza kuwa ulinganifu na mizania ya mitindo hii ni nyenzo muhimu katika kufanikisha mawasiliano ya kisiasa na kuongeza ufanisi wa chombo cha kikatiba.*

***Maneno Muhimu****: Mtindo wa Lugha, Baraza la Wawakilishi Zanzibar (BLW), Nadharia ya Dhima za Lugha, Mawasiliano ya Kisiasa, Isimu Jamii.*

## 1. UTANGULIZI

Lugha ni chombo muhimu kinachofungamanisha mawasiliano na utamaduni katika jamii. Mbali na kutumika kuelezea mahitaji ya kila siku, lugha ni mfumo changamano ambao mwanadamu hujifunza na kuutumia kuwasilisha mawazo, hisia na maoni kulingana na mazingira maalumu ya kijamii ([8], [11], [10]). Kwa mtazamo huo, lugha haiwezi kutazamwa kama bidhaa iliyokamilika, bali ni dhana hai inayobeba maana mbalimbali zinazojidhihirisha kupitia mitindo tofauti ya matumizi kama vile lahaja na rejista [5]. Mitindo hiyo huathiriwa na mazingira, madhumuni ya mawasiliano pamoja na wahusika wanaotumia lugha husika.

Aidha, ufanisi wa mawasiliano hutegemea uwezo wa mtumiaji wa lugha kuendana na muktadha wa matumizi yake. Mtumiaji mwenye umahiri hutambua kuwa lugha ni mfumo unaobadilika kulingana na mahitaji ya mawasiliano na mazingira ya kijamii. Kwa sababu hiyo, matumizi sahihi ya rasilimali za lugha huchangia katika kuwasilisha mawazo, mapendekezo na maamuzi kwa ufanisi ([7], [9], [5]). Hali hii hujitokeza zaidi katika taasisi rasmi ambako lugha hutumika kama nyenzo ya kujenga hoja, kushawishi na kufanikisha maamuzi muhimu ya kijamii na kisiasa.

Kutokana na tofauti za mazingira ya matumizi, taasisi mbalimbali kama skuli, mahakama na vyombo vya kutunga sheria huibua mitindo mahsusi ya lugha. Baraza la Wawakilishi la Zanzibar ni miongoni mwa taasisi zinazodhihirisha matumizi hayo ya lugha kupitia mijadala yake ya kisheria na kisiasa. Katika mijadala hiyo, wajumbe hutumia mitindo mbalimbali ya lugha ili kufafanua hoja, kushawishi, kuelekeza na kusisitiza misimamo yao.

Licha ya kuwepo kwa tafiti mbalimbali zinazohusu lugha na mawasiliano, bado kuna uhaba wa maarifa ya kimfumo kuhusu dhima mahususi za mitindo ya lugha katika mijadala ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar (BLW). Hivyo, makala hii inakusudia kuziba pengo hilo kwa kuchunguza dhima hizo kupitia mwongozo wa Nadharia ya Dhima za Lugha ya [1]. Utafiti huu unalenga kubainisha jinsi mitindo hiyo inavyotumika kama nyenzo ya kimkakati katika kujenga hoja na kuendesha mawasiliano ya kisiasa na kijamii ndani ya Baraza hilo, hivyo kutoa mchango mpya katika uelewa wa rejista za kibunge nchini.

## 2. KIUNZI CHA NADHARIA

Nadharia ya Dhima za Lugha, kama ilivyobainishwa na [1], inashughulika na namna lugha inavyotekeleza majukumu mbalimbali ya kijamii, kisaikolojia, na kiakili. Kulingana na nadharia hii, lugha ni chombo cha mawasiliano kinachowawezesha watu kuwasiliana, kubadilishana mawazo, na kueneza maarifa katika jamii. Hata hivyo, matumizi ya lugha hayapaswi kutenganishwa na muktadha wa kijamii, hadhi za wahusika, na malengo ya mawasiliano, kwani vipengele hivi vinaathiri namna lugha inavyotumika na kufasiriwa. Hivyo basi, misingi ya nadharia ya [1] kama vile lugha kuwa chombo cha mawasiliano, ushawishi, ujengaji wa mahusiano ya kijamii, pamoja na kuakisi mamlaka na utambulisho wa wahusika, inaonekana wazi katika uchambuzi wa matumizi ya lugha ndani ya mijadala ya Baraza la Wawakilishi.

[1] anasisitiza kuwa matumizi ya lugha hupanua dhana ya dhima za lugha kwa kuzingatia jinsi zinavyoakisi hali ya kijamii, kitamaduni, na kimamlaka. Lugha hutumika siyo tu kuwasilisha ujumbe, bali pia kujieleza, kuhamasisha hisia, kushawishi, na kuunda uhusiano wa kijamii. Kwa hivyo, kuelewa matumizi ya lugha kunahitaji kuchunguza madhumuni ya mzungumzaji pamoja na athari za kijamii na kisiasa zinazohusiana na matumizi hayo.

Misingi ya nadharia ya [1] ni pamoja na lugha kuwa chombo cha mawasiliano, lugha kama nyenzo ya ushawishi, lugha katika kujenga mahusiano ya kijamii, pamoja na lugha kuakisi mamlaka na utambulisho wa wahusika. Vilevile, nadharia hii inaeleza kuwa mitindo ya lugha hubadilika kulingana na mazingira, hadhira, na madhumuni ya mawasiliano.

Katika muktadha wa mijadala ya Baraza la Wawakilishi (BLW), nadharia ya Chaika inatoa msingi wa kuchambua matumizi ya lugha na dhima zake katika mawasiliano. Kupitia nadharia hii, tunachunguza jinsi mitindo ya lugha inavyotumika kuwasilisha hoja, kuhamasisha mitazamo, na kudumisha uhusiano wa kijamii na kisiasa.

## 3. METHODOLOJIA

Utafiti huu ulifanyika Chukwani, Zanzibar katika kisiwa cha Unguja, hususan katika Wilaya ya Magharibi 'B', Mkoa wa Mjini Magharibi. Sampuli ilihusisha washiriki ishirini (20), wakijumuisha wajumbe kumi (10) wa Baraza la Wawakilishi (BLW) na waandishi kumi (10) wa Hansadi. Aidha, sampuli ya matini ilihusisha kumbukumbu kumi na mbili (12) za Hansadi zinazohusiana na mikutano

ya Baraza. Mbinu ya usampulishaji wa kimakusudi ilitumiwa kuteua Hansadi hizo kulingana na ukamilifu wa taarifa, uwepo wa vielelezo vya mitindo ya lugha, na uhusiano wake wa moja kwa moja na malengo ya utafiti.

Katika ukusanyaji wa data, utafiti huu ulitumia mbinu ya hojaji ambapo dodoso ilitumika kama zana ya kukusanyia data. Sambamba na hilo, mbinu ya uchambuzi wa matini ilitumika kuchambua kumbukumbu rasmi za mijadala za mijadala ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar (BLW). Matumizi ya mbinu hizi yalikuwa ni kupata data za msingi zinazohusu dhima za mitindo ya lugha katika muktadha wa kijamii na kisiasa.

Uhalali na uwaminifu wa data ulidhibitiwa kupitia matumizi ya hojaji, pamoja na uteuzi wa hansardi kama kumbukumbu rasmi za Baraza la Wawakilishi. Matumizi ya vyanzo hivyo rasmi yalisaidia kuhakikisha upatikanaji wa taarifa sahihi, za kutosha na za kuaminika kwa ajili ya uchambuzi wa utafiti huu.

Data za upili zilipatikana kutoka katika mapitio ya maandiko, makala, na machapisho mbalimbali yanayohusu mitindo ya lugha katika mijadala ya Baraza la Wawakilishi (BLW), hususan katika muktadha wa Kiswahili. Vyanzo hivi vilikusanywa kutoka maktaba za vyuo vikuu na taasisi za kiutafiti ili kutoa uelewa mpana juu ya dhima za mitindo ya lugha katika mawasiliano ya kisiasa.

Baada ya kukusanywa, data hizo zilichambuliwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli. Mkabala huu uliruhusu ufafanuzi wa kina wa kimaelezo badala ya takwimu, ukijikita katika uchambuzi wa matini za kijamii na kisiasa. Nadharia ya Dhima za Lugha ya [1] ilitumika kama mfumo wa kinadharia katika kufafanua madhumuni ya matumizi ya lugha katika mawasiliano kati ya wawakilishi na wananchi wa Zanzibar.

## 4. MATOKEO YA UTAFITI

Sehemu hii inachambua dhima za mitindo ya lugha katika mijadala ya Baraza la Wawakilishi (BLW) kwa kutumia Nadharia ya [1]. Uchambuzi umejikita katika kuonesha jinsi lugha inavyotumika kuwasilisha taarifa, kushawishi hoja, na kudhibiti mtiririko wa mawasiliano ndani ya chombo hicho cha kikatiba.

Data zilizokusanywa kupitia mbinu ya hojaji ambapo dodoso ilitumika kama zana ya kukusanyia data, na uchambuzi wa kumbukumbu rasmi za mijadala zinaonesha kuwa uteuzi wa mitindo ya lugha katika BLW unaongozwa na madhumuni ya washiriki pamoja na muktadha wa majadiliano. Matokeo yanathibitisha kuwa mitindo ya lugha haitumiki kama nyenzo ya mawasiliano pekee, bali ni chombo muhimu cha kujenga mshikamano, kuimarisha nidhamu ya kitaasisi, na kuhalalisha maamuzi ya kiserikali.

### 4.1 Dhima Mahususi za Mitindo ya Lugha katika BLW

Dhima mahususi zinahusiana na mtindo mmoja maalumu wa lugha miongoni mwa mitindo mbalimbali inayotumika katika BLW. Mitindo hiyo, kama tulivyokuwa tumeibainisha hapo awali, ni mtindo rasmi, mtindo wa mashauriano, mtindo wa kawaida, na mtindo usiobadilika, ambapo kila mmoja una jukumu maalumu katika kuunda, kueleza, na kuendeleza mawasiliano ya kisiasa ndani ya BLW.

#### 4.1.1 Dhima za Mtindo Usiobadilika katika Mijadala ya BLW

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa, katika mijadala ya BLW, hujitokeza mitindo mbalimbali ya matumizi ya lugha yenye dhima tofauti kulingana na muktadha wa matumizi. Kupitia data za dodoso na uchambuzi wa mijadala, utafiti uligundua kuwa miongoni mwa mitindo inayoonekana kwa uwazi ni mtindo wa lugha usiobadilika, unaotumika katika mazingira rasmi ya uendeshaji wa shughuli za Baraza. Mtindo huu hujitokeza katika vipengele vya lazima vya kikao kama dua, Wimbo wa Taifa, marejeo ya kikanuni na kauli za kitaratibu.

##### 4.1.1.1 Kuimarisha Utambulisho wa Kitaifa

Uchambuzi umeonesha kuwa mtindo usiobadilika hutumika hasa katika vipengele vya lazima vya uendeshaji wa kikao, hususan katika dua na Wimbo wa Taifa kabla ya kuanza kwa mijadala. Kwa mfano, katika Data Na. 1, dua huanza kwa kauli: *"Tunakuomba Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, bwana wa viumbe vyote, uiweke nchi yetu ya Zanzibar…"* na kuhitimishwa kwa kauli ya pamoja *"Twakuomba utupe hekima na busara, sisi wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar … Amin."* Mtindo huu hutamkwa kwa mtiririko uleule katika kila kikao bila mabadiliko ya kimuundo au kimaudhui. Kutokana na ushahidi huu, uchambuzi umeonesha kuwa mtindo usiobadilika hutekeleza dhima ya kuimarisha utambulisho wa kitaifa, kuamsha hisia za uzalendo na mshikamano, pamoja na kuwaandaa kisaikolojia wajumbe kwa ajili ya mijadala. Mhojiwa mmoja alieleza, *"Dua na Wimbo wa Taifa ni sehemu ya lazima ya kikao na hubeba maadili ya umoja na uzalendo."* Hali hii inaonesha kuwa lugha hiyo huwaandaa kisaikolojia wajumbe na kuipa mijadala mwelekeo wa nidhamu na heshima.

##### 4.1.1.2 Kuimarisha Nidhamu na Kudhibiti Mtiririko wa Mawasiliano

Vilevile, mtindo huu hujitokeza katika kauli rasmi za wajumbe wanapoomba nafasi ya kuchangia au kujibu hoja. Mfano katika Data Na. 3 hujitokeza kauli, *"Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba…", "Naomba kutoa taarifa kwamba miswada…" na "Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali…"*. Kauli hizi hurudiwa kwa mtindo uleule katika kila kikao na haziwezi kubadilishwa kiholela. Hali hii hudhibiti mtiririko wa mawasiliano na kuimarisha heshima kwa mamlaka ya uongozi wa Baraza. Mhojiwa mmoja alisema, *"Maneno haya ni lazima yatumike; huwezi kuanza kuzungumza bila kuyasema."*

#### 4.1.1.3 Kuhalalisha Taratibu za Kisheria

Aidha, utafiti ulibaini kuwa mtindo huu hujitokeza katika matamko ya Spika au Mwenyekiti wanaporejea kanuni za Baraza. Kwa mfano, katika Data Na. 2 hutolewa kauli *"Kama inavyotakiwa chini ya Kanuni ya 92(3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020…"* kwa mtindo usiobadilika unaotokana moja kwa moja na maandiko ya kanuni. Mhojiwa mmoja alieleza, akisema, *"Spika hutumia maneno yaleyale yanayotokana na kanuni ili kuonesha kuwa maamuzi yote yanazingatia sheria."* Ushahidi huu unaonesha kuwa lugha isiyobadilika hutekeleza dhima ya kuhalalisha taratibu za Baraza, kuimarisha mamlaka ya uongozi na kudumisha uhalali wa kisheria wa maamuzi yanayofanywa.

Zaidi ya hayo, lugha isiyobadilika hutumika katika uwasilishaji wa taarifa za kifedha na marejeo ya kisheria. Kwa mfano, katika Data Na. 4, kunatajwa vipengele vya bajeti kama vile *"Kifungu C010 - Ofisi Kuu Pemba 22,542,000/="* na *"Jumla ya Fungu 26,000,200,000/="*. Aidha, katika Data Na. 5 kuna marejeo mahususi ya kisheria kama vile *"Sheria ya Kudhibiti Vileo Nam. 9 ya mwaka 2020… kwa kuzingatia kifungu cha 33(1)."* Miundo hii haiwezi kubadilishwa bila kupotosha maana au kuvuruga usahihi wa kisheria na kifedha, hivyo, kuonesha kuwa mtindo usiobadilika hulinda usahihi na uhalali wa taarifa rasmi. Hata katika hotuba za kidini au ufunguzi wa kikao, kama inavyoonekana katika Data Na. 6 *"Sifa njema zote zinamstahikia Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehema …"*, muundo hubaki uleule kwa kila kikao, jambo linalothibitisha tabia ya kurudiarudia ya mtindo huu.

Kwa jumla, ushahidi wa data unaonesha kuwa mtindo wa lugha usiobadilika katika BLW una dhima muhimu za kuimarisha utambulisho wa kitaifa, kuamsha hisia za mshikamano, kuhalalisha taratibu za kisheria, kudhibiti mtiririko wa mjadala na kulinda usahihi wa taarifa rasmi. Hivyo basi, mtindo huu si utaratibu wa lugha tu, bali ni nyenzo ya kitaasisi inayochangia uhalali, nidhamu na ufanisi wa mawasiliano ya kisiasa ndani ya BLW.

Matokeo haya yanafanana na hoja za [1] katika Nadharia ya Dhima za Lugha, zinazoeleza kuwa, katika taasisi rasmi, lugha hutumika si tu kuwasilisha taarifa bali pia kuhalalisha mamlaka, kudhibiti mwenendo wa mawasiliano na kuunda uhalisia wa kijamii. Aidha, yanaendana na uchambuzi wa [2] kuhusu dhima ya lugha katika taasisi, ambapo anaonesha kuwa mitindo ya lugha inayojirudia huchangia kuimarisha mamlaka, uhalali na uthabiti wa taratibu za kiutawala.

### 4.1.2 Dhima za Mtindo Rasmi katika Mijadala ya BLW

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa mtindo rasmi hutumika katika mijadala ya kisheria, kiutawala na kifedha. Mtindo huu unadhihirika katika taarifa za Spika, michango ya wajumbe, hoja za viongozi wa Serikali na uwasilishaji wa nyaraka rasmi za Baraza kama inavyooneshwa katika Data Na. 7 – 13.

#### 4.1.2.1 Kuhalalisha Taratibu na Maamuzi ya Kisheria

Uchambuzi umebaini kuwa mtindo rasmi hutekeleza dhima muhimu ya kuhalalisha taratibu na maamuzi ya Baraza kisheria na kikatiba. Matumizi ya mtindo huu huambatana na uteuzi makini wa msamiati wa kisheria na kikanuni, miundo ya sentensi iliyo sanifu, pamoja na matumizi ya istilahi zinazotambulika katika muktadha wa taasisi za kiserikali. Kwa kufanya hivyo, lugha inayotumika haibaki kuwa chombo cha mawasiliano pekee, bali hugeuka kuwa nyenzo ya kuidhinisha na kuthibitisha uhalali wa hatua na maamuzi yanayochukuliwa. Aidha, mtindo rasmi huimarisha mamlaka ya kiti cha uongozi, hususan Spika, kwa kuweka bayana mipaka ya kiutaratibu na kuongoza mwenendo wa mjadala kwa mujibu wa kanuni zilizowekwa. Hali hii huchangia kujenga utii, nidhamu, na uhalali wa kisheria miongoni mwa washiriki wa mjadala. Kwa mfano, katika Data Na. 7, Spika anasema:

> *"Kama inavyotakiwa chini ya Kanuni ya 92(3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020; naomba kutoa taarifa kwamba miswada hiyo niliyoitaja, sasa imekuwa sheria kamili baada ya kusainiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi."*

Marejeo haya ya moja kwa moja ya kanuni na mamlaka ya Rais yanaonesha kuwa maamuzi ya Baraza yanafungamanishwa na msingi wa kisheria. Hivyo, hapa, lugha rasmi inatoa uzito wa kikatiba na kuhalalisha hatua zilizochukuliwa. Mhojiwa mmoja alieleza, *"Spika anapotaja kanuni, anatoa uzito wa kisheria kwa maamuzi yanayofanywa na Baraza."* Kauli hii inaonesha kuwa lugha rasmi huimarisha mamlaka na uhalali wa taasisi kwa kuhusisha maamuzi na misingi ya sheria na kanuni.

#### 4.1.2.2 Kudumisha Itifaki, Heshima, na Mpangilio wa Mijadala

Aidha, uchambuzi umeonesha kuwa mtindo rasmi wa lugha hutekeleza dhima ya kudumisha itifaki, heshima na mpangilio wa mijadala. Kauli, kama inavyoonekana katika Data Na. 8, ina muundo maalumu unaotambulika na unaorudiwa katika vikao. Vilevile, katika Data Na. 9, matumizi ya miito kama *"Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Wawakilishi, Mhe. Mwakilishi, Mhe. Spika na Baraza lako Tukufu"* yanaashiria utambuzi wa hadhi za wahusika na kuimarisha heshima ya taasisi. Mhojiwa mmoja alisema, *"Lugha rasmi ni lazima itumike ili kuheshimu mamlaka ya Spika na Mwenyekiti."* Hivyo basi, lugha rasmi hutumika kama chombo cha kudhibiti mienendo ya mawasiliano na kuhakikisha kuwa taratibu za kikao zinafuatwa ipasavyo.

#### 4.1.2.3 Uwasilishaji wa Hoja Kikanuni

Vilevile, imebainika kuwa lugha rasmi hutekeleza dhima ya kuwasilisha hoja, maombi na mapendekezo ya kisera kwa namna inayokubalika kikanuni. Kwa mfano, hoja ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais, kama inavyoonekana katika Data Na. 11, inayosomeka, *"naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu lipokee, lijadili na hatimaye likae kama Kamati ya Mapato na Matumizi ili liidhinishe Makadirio ya Mapato na Matumizi…"* inaonesha matumizi ya vitenzi vya kisheria kama "*lipokee," "lijadili," "liidhinishe,*" vinavyoashiria hatua rasmi za kikanuni. Mhojiwa mmoja alieleza, akisema, *"Hoja za bajeti lazima zitolewe kwa lugha rasmi ili zipokelewe na Baraza."* Kauli hii inaonesha kuwa lugha rasmi ni nyenzo muhimu katika kufanikisha mchakato wa maamuzi na kuhakikisha hoja zinajadiliwa kwa misingi ya kikanuni.

#### 4.1.2.4 Kuonesha Nidhamu na Ufuataji wa Taratibu

Uchambuzi umebaini kuwa, katika Data Na. 10, kauli inaonesha msemaji anaanza kwa shukrani: *"Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuweza na mimi kunipa fursa ili niweze kuchangia hoja …"* Kauli hii inaonesha nidhamu na ufuataji wa utaratibu wa kuomba na kushukuru kabla ya kuwasilisha mchango, jambo linalodhihirisha urasmi wa mawasiliano ya BLW.

Zaidi ya hayo, lugha rasmi hutumika katika kuuliza na kuhoji kwa njia yenye staha na ufanisi. Kama inavyoonekana katika Data Na. 13, mjumbe anasema, *"Ahsante Mhe. Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mhe. Waziri …, lakini pamoja na hayo, nilikuwa nataka kufahamu zaidi. Je, mafunzo haya … yalikuwa yanahusiana na nini? …"* Hapa, kuna mpangilio wa pongezi, ufunguzi wa hoja na swali linalowasilishwa kwa staha, jambo linaloonesha kuwa hata hoja za ukosoaji au ufuatiliaji hutolewa kwa lugha rasmi yenye nidhamu. Mhojiwa mmoja alisema, *"Hata unapouliza swali gumu, lazima utumie lugha rasmi ili lisitafsiriwe vibaya."* Hali hii inaonesha kuwa lugha rasmi husaidia kuibua hoja, kuimarisha uwajibikaji na kudumisha heshima katika mawasiliano ya kibunge.

Kwa kuhusianisha matokeo haya na hoja za [1] kuhusu dhima za lugha, inadhihirika kuwa mtindo rasmi wa lugha katika BLW hauishii kuwa chombo cha mawasiliano pekee, bali hutekeleza kwa kiwango kikubwa dhima za kijamii na kisiasa. Kwa upande wa kijamii, mtindo huu huakisi na kudumisha hadhi za wahusika kwa kuonesha tofauti za kimamlaka na nafasi zao ndani ya taasisi, kama vile kati ya Spika, mawaziri na wajumbe. Matumizi ya lugha yenye heshima, miundo sanifu ya sentensi na istilahi rasmi huchangia kujenga utambulisho wa kitaasisi na kuimarisha nidhamu ya majadiliano.

Aidha, kwa upande wa kisiasa, mtindo rasmi husaidia kuimarisha mamlaka ya viongozi na kuhalalisha maamuzi yanayofanywa ndani ya Baraza kwa kuyafungamanisha na misingi ya kisheria na kikatiba. Kupitia matumizi ya marejeo ya kanuni, taratibu na mamlaka ya juu ya uongozi, lugha hii hujenga uhalali wa maamuzi mbele ya washiriki na hadhira pana. Hivyo basi, kwa mujibu wa mtazamo wa [1], lugha katika muktadha huu inaonekana wazi kuwa ni nyenzo ya kudhibiti mahusiano ya kijamii na kuendeleza nguvu za kisiasa ndani ya taasisi.

Aidha, jambo hili linashabihiana na mtazamo wa [4] katika nadharia ya *Systematic Functional Linguistics* unaoeleza kuwa lugha rasmi katika taasisi hutumika kudumisha nidhamu, mamlaka, uhalali na mpangilio wa kijamii. Mtindo rasmi wa BLW unaonesha kazi hizi kupitia matumizi ya lugha ya kisheria, kiutawala na kifedha, jambo linalolingana na matokeo ya nadharia hiyo ya [4]. Vilevile [12] anaongeza kuwa, katika taasisi, lugha rasmi hujenga na kudumisha nafasi za mamlaka, hali inayodhihirika katika matumizi ya miito ya heshima kama *"Baraza lako Tukufu"* na marejeo ya kikanuni kama *"Kanuni ya 92(3)"*.

Kwa jumla, data za utafiti zilizokusanywa zinaonesha kuwa mtindo rasmi katika mijadala ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar (BLW) si suala la umbo la lugha pekee, bali ni chombo madhubuti cha kitaasisi. Mtindo huu hutekeleza dhima ya kuhalalisha mamlaka, kudumisha itifaki, kuwasilisha hoja

za kisheria na kifedha, na kuhakikisha mijadala inaendeshwa kwa nidhamu na uhalali wa kikatiba. Hivyo basi, mtindo rasmi ni nyenzo muhimu katika kuimarisha utendaji, ufanisi na uhalali wa taasisi ya BLW ndani ya mfumo wa utawala wa kidemokrasia, ukichangia kwa kiasi kikubwa katika kuendeleza mawasiliano yenye tija na uthabiti wa kiutawala.

#### 4.1.3 Dhima za Mtindo wa Mashauriano katika Mijadala ya BLW

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa, mtindo wa mashauriano hujitokeza kwa kiwango kikubwa katika mijadala ya BLW hususani pale wajumbe wanapotoa maelezo, kushauri, kujibu hoja au kuhimiza ushirikiano katika utekelezaji wa maamuzi ya maendeleo. Data zinaonesha kuwa mtindo huu una dhima mahususi za kijamii, kiutendaji na kisiasa ndani ya Baraza.

#### 4.1.3.1 Kuimarisha ushirikiano wa Kitaasisi na Kijamii

Uchambuzi unaonesha kuwa mtindo wa mashauriano hutekeleza dhima ya kuhimiza ushirikiano wa kitaasisi na kijamii. Katika Data Na. 14, msemaji anasema,*"Tunaendelea kushirikiana na taasisi zote za Serikali…* Sisi tunavihifadhi vizuri, tunawapatia ili waendeleze hiyo historia…"

Matumizi ya viwakilishi vya nafsi ya kwanza wingi kama "*tunaendelea,*" "*sisi*," na "*tunawapatia"* yanaonesha uwajibikaji wa pamoja kati ya taasisi za Serikali. Aidha, katika Data Na. 16 msemaji anaeleza, *"Tutahitaji mashirikiano makubwa kutoka kwa wananchi …* ili kuweza kukamilisha jambo hilo."

Kauli hizi zinaashiria matumizi ya lugha inayojenga mshikamano kati ya Serikali, Baraza na wananchi katika kufanikisha utekelezaji wa maamuzi. Hivyo, hapa, lugha ya mashauriano inajenga taswira ya umoja, mshikamano na ushirikiano badala ya mamlaka ya upande mmoja. Ushahidi wa dodoso unaimarisha hoja hii, hasa pale mhojiwa mmoja alipoeleza, akisema, *"Lugha ya mashauriano huwafanya wajumbe waone kuwa Serikali iko tayari kusikiliza na kushirikiana nao badala ya kutoa maamuzi kwa upande mmoja."* Mhojiwa mwingine aliongeza, *"Unaposema 'tunaendelea kushirikiana', unajenga picha ya umoja na uwajibikaji wa pamoja."* Kutokana na ushahidi huu, mtindo wa mashauriano huimarisha uhusiano wa kitaasisi na kijamii katika muktadha wa mijadala ya BLW.

#### 4.1.3.2 Kutoa Ushauri

Utafiti ulibaini kuwa mtindo wa mashauriano hutumika kutoa ushauri na mapendekezo kwa namna ya kujenga. Katika Data Na. 15 kamati inasema, *"Kamati inashauri kuwa ni muhimu kuhakikisha miradi ya ajira za muda… Aidha, tunapendekeza kuweka mikutano ya kila mwezi* ili kusikiliza changamoto za walengwa …"

Matumizi ya vitenzi "*inashauri"* na "*tunapendekeza"* yanaonesha kuwa hoja zinawasilishwa kwa mtazamo wa kujenga na kushirikisha badala ya maelekezo ya moja kwa moja. Ushahidi wa dodoso unaonesha kuwa m*tindo wa mashauriano hutoa nafasi ya kutoa mapendekezo bila kuonekana kama*

*unapingana moja kwa moja na Serikali.* Hivyo, lugha ya mashauriano hurahisisha mchakato wa maboresho ya kiutendaji na kuimarisha ufanisi wa utekelezaji wa maamuzi ya Baraza.

**4.1.3.3 Ushirikishwaji wa Wananchi**

Utafiti ulibaini kuwa mtindo wa mashauriano una dhima ya kuwahusisha wananchi katika mchakato wa maamuzi. Katika Data Na. 16, msemaji anasema,, " *…nikujibu swali lako kwa niaba ya wananchi wa Kojani … ."*

Kauli hii inaonesha uwakilishi wa moja kwa moja wa wananchi ndani ya Baraza, jambo linaloimarisha dhana ya ushirikishwaji na uwajibikaji wa viongozi kwa jamii. Hii ni dhima ya msingi ya mtindo wa mashauriano, kwani unajenga hisia kwamba wananchi wanashirikishwa katika mchakato wa kisiasa na utawala, na kwamba maamuzi yanayofanywa yanahusisha pande zote.

**4.1.3.4 Kudumisha Mahusiano ya Kijamii**

Utafiti ulibaini kuwa mtindo wa mashauriano hutekeleza dhima ya kuimarisha mahusiano na kupunguza migongano katika mijadala. Katika Data Na. 17, mjumbe anaanza kwa pongezi na heshima "Ahsante sana Mhe. Spika, nampongeza sana Mhe. Waziri…" kabla ya kuwasilisha hoja *"lakini naomba nimpe taarifa tu kwamba tatizo hili haliko Kombeni na Maungani tu…"* Mpangilio huu unaonesha mkakati wa kuwasilisha changamoto kwa lugha ya staha ili kupunguza mvutano na kuimarisha mawasiliano ya kujenga. Mhojiwa mmoja alieleza kuwa: *"Kuanza kwa pongezi hupunguza mvutano na kufanya mjadala uwe wa staha."*

Katika Data Na. 18, kauli kama *"bila shaka viongozi wetu wote hawa wameonesha uwezo mkubwa …"* na *"Namuomba Mwenyezi Mungu awazidishie uwezo na hekima …"* zinaonesha mshikamano na kuimarisha uhusiano wa kijamii katika muktadha rasmi. Huu ni mtindo unaochanganya heshima na ushirikishwaji, ambapo viongozi wanaonesha kuwa wanathamini na kuenzi michango ya wenzao na wananchi.

Data Na. 19 inaonesha utoaji wa taarifa kwa namna inayoruhusu mjadala zaidi: *"Kampuni ya Novavis kutoka Marekani inakamilisha utafiti …"* Uwasilishaji huu unaonesha uwazi na uwezekano wa kupokea maoni ya ziada kuhusu maendeleo ya mradi. Katika Data Na. 20, msemaji anasema, *"Tuna programu kubwa ya upandaji wa miti ambayo inaitwa Zanzibar Green Legacy Program …"* Matumizi ya neno "*tuna"* yanaashiria umiliki wa pamoja na ushirikishwaji wa taasisi na jamii katika utekelezaji wa programu hiyo.

Vilevile, Data Na. 21 inaonesha mchakato wa kujenga mahusiano chanya kati ya Serikali na wadau kupitia kauli *"Wizara inawaenzi kwa kuwasaidia kifedha, kuwasaidia studio za kurekodi bila tozo …."*.Hapa, kuna mfuatano wa vitenzi *"kuwasaidia…" "kuwapatia…"* vinavyoashiria hatua za kuimarisha ushirikiano. Katika Data Na. 22, kauli *"Kazi za wabunifu hawa, wakiwamo watu wenye ulemavu ni nyingi na tumezipokea"* pamoja na *"ubunifu wao una matokeo chanya kwa jamii"* zinaonesha kukubali na kuthamini mchango wa wadau. Matumizi ya *"tumezipokea"* yanaonesha

hatua ya pamoja ya taasisi kutambua mchango huo, jambo linaloimarisha mashauriano na ushirikishwaji. Ushahidi wa dodoso, unaunga mkono hoja hii kwa kuonesha kuwa *“Lugha ya mashauriano huwafanya wananchi wajisikie kuwa wao ni sehemu ya maamuzi yanayofanyika ndani ya Baraza.”*

Kwa kuhusianisha matokeo haya na hoja za [1] kuhusu dhima za lugha, mtindo wa mashauriano katika BLW unatekeleza dhima ya kijamii ya kujenga mshikamano na kudumisha mahusiano baina ya washiriki. Aidha, kwa mujibu wa [3], lugha hutumika kuunda mahusiano ya kijamii, jambo linalodhihirika wazi katika matumizi ya kiwakilishi jumuishi “tu” kama kilivyotumika katika vitenzi *“tuna,” “tutahitaji,”* na *“tumezipokea*.” Mtazamo wa Wodak pia unaonesha kuwa, katika taasisi, lugha hutumika kujenga makubaliano na kuimarisha ushiriki wa wadau, hali inayoonekana katika data hizi.

Kwa jumla, kwa kuzingatia ushahidi wa data za utafiti pamoja na maoni ya wahojiwa, mtafiti anahitimisha kuwa mtindo wa mashauriano katika BLW unaonesha dhima ya kuhimiza ushirikiano, kutoa ushauri wa maboresho, kuwahusisha wananchi na kudumisha mahusiano mazuri katika mijadala. Mtindo huu si utaratibu wa lugha pekee bali ni nyenzo ya kimkakati inayochangia ufanisi wa mawasiliano ya kisiasa, ujenzi wa maridhiano na utekelezaji bora wa sera ndani ya BLW.

Matokeo haya yanalandana na matokeo ya [3] anayebainisha kuhusu dhima za lugha zinazohusiana na mwingiliano wa kijamii na mawasiliano ya kibinafsi, ambapo lugha hutumika kuanzisha mawasiliano, kutoa ushauri na kushirikisha mawazo kwa namna inayoimarisha mshikamano na heshima miongoni mwa washiriki.

#### 4.1.4 Dhima za Mtindo wa Kawaida katika Mijadala ya BLW

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa mtindo wa kawaida hujitokeza kwa uwazi katika mijadala ya BLW. Uchambuzi wa data pamoja na ushahidi wa dodoso unaonesha kuwa mtindo huu hutekeleza dhima mbalimbali za kijamii, kimawasiliano na kisaikolojia katika muktadha wa mijadala ya BLW. Tofauti na mitindo rasmi na ya mashauriano, mtindo wa kawaida hujengwa juu ya lugha ya mazungumzo ya kila siku, tashbihi, sitiari, utani na uzoefu binafsi.

##### 4.1.4.1 Kurahisisha Uelewa wa Hoja

Uchambuzi wa Data Na. 25 na 27 unaonesha matumizi ya tashbihi na semi za kawaida katika kuwasilisha hoja. Kwa mfano, katika Data Na. 25, mjumbe anasema, *“Niwaombe tu kwamba tupitisheni bajeti hii bila lolote. hii ni kama kumsukuma mlevi … ,”* Kauli hii inatumia tashbihi inayotokana na uzoefu wa maisha ya kila siku (hii ni kama kumsukuma mlevi) ili kujenga taswira inayoeleweka kwa urahisi mbele ya hadhira. Vilevile, katika Data Na. 27, mjumbe anasema, *“Hii Sheria tukiingiza kila kitu humu itakuwa mchuzi wa wale jamaa zetu … .”*

Kauli hii inatumia sitiari ya *mchuzi* kuashiria mkusanyiko usio na mpangilio maalumu. Matumizi haya ya lugha ya kawaida hurahisisha hoja nzito za kisheria au kisera kwa kuziweka katika muktadha wa uzoefu wa kila siku wa jamii unaotambulika kirahisi.

Mtindo huu hutekeleza dhima ya kurahisisha uelewa kwa kuibua taswira zinazotokana na mazingira ya kijamii ya hadhira. Ushahidi wa dodoso unaunga mkono hoja hii, ambapo mhojiwa mmoja alieleza, *"Wakati mwingine, tunatumia mifano ya kawaida ili watu waelewe hoja nzito kwa haraka."*

Uchambuzi huu unaonesha kuwa mtindo wa kawaida katika mijadala ya BLW si tu chombo cha mapambo ya lugha, bali ni mkakati wa kimawasiliano unaolenga kuongeza uelewa, kuvutia usikivu wa hadhira, na kuimarisha uzito wa hoja zinazowasilishwa.

**4.1.4.2 Kujenga Ukaribu wa Kijamii**

Data Na. 24 na 29 zinaonesha namna wajumbe wanavyoingiza uzoefu binafsi au mazungumzo ya moja kwa moja yanayofanana na lugha ya mitaani. Katika Data Na. 24, mjumbe anasema, *"Mimi nashukuru sana watu hawa kudai kwa mfumo huo, lakini wangekuja nyumbani kwangu wakanidai sijui ingekuwaje. Nisingekubali hata siku moja."*

Mtindo huu hutekeleza dhima ya kujenga ukaribu kati ya mjumbe na hadhira. Mhojiwa mmoja alieleza, *"Lugha ya kawaida humsaidia mjumbe kuzungumza kama anavyoongea na wananchi wake."* Hali hii huimarisha taswira ya mjumbe kama mwakilishi anayeshirikiana na wananchi, badala ya kuonekana kama kiongozi aliye mbali na jamii. Vilevile, katika Data Na. 29, waziri anasema, *"Wale wakija wanakuja na vyeti vyao, wale waganga tena utashangaa, kuna mababa waganga hapa."*

Kauli hii inaiga mtindo wa mazungumzo ya kila siku, ikijumuisha mtiririko wa usemi usio rasmi unaoweza kuibua hisia na taswira za moja kwa moja kwa wasikilizaji. Lugha ya aina hii hujenga athari ya ukaribu na ushirikishwaji kwani hadhira hutambua mitindo hiyo kama sehemu ya mawasiliano yao ya kawaida.

Kwa jumla, matumizi ya lugha ya mazungumzo ya moja kwa moja katika mijadala ya BLW yana dhima ya kuondoa umbali kati ya lugha ya taasisi na lugha ya jamii. Hivyo, mtindo wa kawaida unakuwa nyenzo muhimu ya kuimarisha mawasiliano, kuongeza mvuto wa hoja, na kujenga uhusiano wa karibu kati ya wazungumzaji na hadhira yao.

**4.1.4.3 Kupunguza Mvutano katika Mijadala**

Uchambuzi wa Data Na. 23 na 28 unaonesha matumizi ya utani na vicheko kama sehemu ya mtindo wa kawaida unaolenga kupunguza mvutano na kuleta uhai katika mjadala. Kwa mfano, katika Data Na. 23 mjumbe anasema, *Mhe. X anaishi majimbo mawili na ndio maana nikawa kidogo nasitasita (kicheko),"*

Uwapo wa maelezo *(kicheko)* unaonesha kuwa kauli hiyo ilipokelewa kwa hali ya mzaha hivyo, kupunguza uzito wa hoja na kuondoa uwezekano wa kuibua mvutano wa moja kwa moja. Kadhalika, katika Data Na. 28, Spika anasema,*"Haya makofi maalumu kwa mwenza yana maana yake ambayo Mhe. Mwakilishi mwenyewe atakuja kuwaelezea."*

Kauli hii ina ladha ya mzaha ndani ya muktadha rasmi. Kwa mujibu wa ushahidi wa dodoso, *mzaha kidogo unasaidia kupunguza joto la mjadala hasa pale hoja zinapokuwa kali.* Kauli hii inaonesha kuwa utani hutekeleza dhima ya kisaikolojia ya kudhibiti hisia na kuimarisha mazingira ya maelewano ndani ya kikao.

Kwa jumla, matumizi ya utani katika mijadala ya BLW hutekeleza dhima ya kisaikolojia kwa kusaidia kudhibiti hisia, kupunguza ukali wa hoja, na kuimarisha mazingira ya maelewano. Aidha, huimarisha mshikamano wa kijamii miongoni mwa wajumbe kwa kuunda hali ya ushiriki isiyo na mkazo mkubwa wa kimvutano.

#### 4.1.4.4 Kufikisha Ujumbe kwa Uwazi

Data Na. 26 inaonesha matumizi ya lugha rahisi na ya mazungumzo katika kuwasilisha taarifa ya kiutendaji kupitia kauli "Mheshimiwa sasa hivi Serikali inao mpango mwengine wa kujenga kiwanda cha mwani ambao haupandwi." Mtindo huu hutekeleza dhima ya kufikisha ujumbe kwa uwazi bila kuathiri heshima ya msingi ya kikao. Hata hivyo, mhojiwa mmoja alionya kuwa, *"Lugha ya kawaida ikizidi sana inaweza kupunguza uzito wa hoja."* Kauli hii inaonesha kuwa, ingawa mtindo wa kawaida una faida za kimawasiliano, matumizi yake yanahitaji mizania ili kulinda hadhi ya taasisi.

Kwa kuzingatia Data za utafiti zilizokusanywa pamoja na ushahidi wa dodoso, inaonekana kuwa mtindo wa kawaida katika BLW hutekeleza dhima za kuvutia hadhira, kurahisisha uelewa wa hoja, kujenga ukaribu wa kijamii, na kupunguza mvutano katika mijadala. Kwa mujibu wa mkabala wa dhima za lugha katika muktadha wa kijamii [1], lugha inapoweza kuamsha hisia na kuleta taswira zinazoeleweka kirahisi, huongeza ufanisi wa mawasiliano. Kwa mantiki hiyo, mtindo wa kawaida katika BLW ni nyenzo muhimu ya kimawasiliano, mradi utumike kwa kuzingatia mipaka ya kitaasisi na matarajio ya heshima ya chombo cha kikatiba.

Hata hivyo, mitazamo ya [4] na [6] inaweka mkazo zaidi katika dhima za kijamii, kiutendaji na kimuundo za lugha katika mazingira rasmi ya kitaasisi. Kwa mantiki hiyo, mtindo wa kawaida katika BLW unaonekana kupanua mipaka ya lugha rasmi kwa kuingiza vipengele vya kijamii na kisaikolojia vinavyoongeza uhai wa mjadala.

## 5. HITIMISHO

Makala hii ilichunguza dhima za mitindo ya lugha katika mijadala ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar (BLW) kwa kuongozwa na Nadharia ya Dhima za Lugha ya Elaine Chaika. Utafiti ulilenga kubainisha namna mitindo mbalimbali ya lugha inavyotumika katika kuwasilisha hoja, kuhalalisha mamlaka, kuimarisha mahusiano ya kijamii, na kurahisisha mawasiliano ya kisiasa ndani ya Baraza.

Katika kufanikisha lengo hilo, utafiti ulitumia mbinu ya hojaji kwa kutumia dodoso kama zana ya ukusanyaji wa data, sambamba na uchambuzi wa matini za kumbukumbu rasmi kumi na mbili (12) za Hansard. Aidha, sampuli ya utafiti ilihusisha washiriki ishirini (20), waliowajumuisha wajumbe kumi (10) wa BLW pamoja na waandishi kumi (10) wa Hansard.

Matokeo ya utafiti yameonesha kuwa matumizi ya mitindo ya lugha katika BLW si ya nasibu, bali hutegemea muktadha wa mawasiliano, madhumuni ya hoja, na hadhi ya washiriki wa mjadala. Utafiti umebainisha mitindo mikuu minne ya lugha (usiobadilika, rasmi, mashauriano, na kawaida), ambapo kila mmoja una dhima mahususi katika uendeshaji wa shughuli za Baraza. Mtindo usiobadilika huimarisha utambulisho wa kitaifa na kuhalalisha taratibu za kisheria; mtindo rasmi hudumisha itifaki, heshima, na uhalali wa maamuzi ya kiserikali; mtindo wa mashauriano huimarisha ushirikiano wa kitaasisi na ushirikishwaji wa wananchi; huku mtindo wa kawaida ukirahisisha uelewa wa hoja, kujenga ukaribu wa kijamii, na kupunguza mvutano katika mijadala.

Kwa ujumla, utafiti umeonesha kuwa lugha ni mhimili muhimu wa mawasiliano ya kisiasa na kiutawala katika BLW, kwani hutekeleza dhima za kijamii, kisiasa, na kiitikadi katika kuimarisha uwajibikaji, mshikamano wa kijamii, na uhalali wa taasisi za uwakilishi. Hivyo basi, matumizi sahihi na yenye mizania ya mitindo ya lugha ni nyenzo muhimu katika kuimarisha ufanisi wa Baraza la Wawakilishi pamoja na kukuza mawasiliano bora kati ya viongozi na wananchi.

**MAREJELEO**


[1] Chaika, E. (1982). *Language: The society mirror*. New House Publisher.

[2] Fairclough, N. (1989). *Language and power*. Longman.

[3] Halliday, M. A. K. (1973). *Explorations in the functions of language*. Edward Arnold.

[4] Halliday, M. A. K. (1978). *Language as social semiotic*: The social interpretation of language and meaning. Edward Arnold.

[5] King'ei, K. (2010). *Misingi ya Isimujamii*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

[6] Leech, M. (1977). *Five Functions of Language*. London: Longman.

[7] Luvai, A. (1991). Poetry through a popular medium. In K. Sanam & D. Williams (Eds.), *Poetry studies* (pp. 1–12).

[8] Lyons, J. (1981). *Language and linguistics*. Cambridge University Press.

[9] Mghambi, S. (1991). *Ukiushi katika lugha ya kimaongezi dhidi ya kanuni za Kiswahili sanifu*. [Unpublished master's thesis]University of Nairobi.

[10] Sapir, E. (1921). Language: *An introduction to the study of speech.* Harcourt, Brace & World.

[11] Wardaugh, R. (2006). *An introduction to sociolinguistics* (5th ed.). Blackwell Publishing.

[12] Wodak, R., & Meyer, M. (Eds.). (2001). *Methods of critical discourse analysis*. Sage Publications.